



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA



SALAMU ZA RAMBIRAMBI

Tunduma, Tarehe 10 Februari 2024.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Tunduma, Mariam Chaurembo kwa niaba ya Baraza la Madiwani, Menejimenti, Watumishi na Wananchi wote wa Mji wa Tunduma, amepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha aliyewahi kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2005 hadi 2008, Mhe. Edward Ngoyai Lowassa kilichotokea leo Tarehe 10 Februari 2024 katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete alipokuwa akipatiwa matibabu.

Mhe. Lowassa alikuwa akisumbuliwa na matatizo ya mapafu na shinikizo la damu hadi alipofariki dunia.

Marehemu Edward Ngoyai Lowassa kwa nyakati tofauti amelitumikia taifa la Tanzania katika nyadhifa mbalimbali ambapo wakati wa uhai wake, amewahi kuwa Waziri wa Maji na Mifugo mwaka 2000 hadi 2005 na baadaye kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2005 hadi 2008.

Chaurembo, amesema Halmashauri ya Mji Tunduma inaitakia familia ya Marehemu Lowassa, ndugu na marafiki moyo wa Subira katika kipindi hiki kigumu cha maombolezo na anamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, Amin.


Benton J. Nollo

Mkuu Wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Mji Tunduma